

5. Vituo vya afya ya jamii

Kuna vituo vya afya ya jamii vya Queensland vinvyopatikana katika kila maeneo ya Wilaya ya Huduma ya Afya, kila kituo kikihudumia jamii ya mitaa. Aina za huduma zinazopatikana kwa kila kituo cha afya ya jamii ni tofauti, hizi huonyesha mahitaji tofauti kulingana na matakwa tofauti ya jamii ya mitaa.

Ili kupata kituo cha afya ya jamii kilicho karibu na wewe, piga simu ya 13HEALTH nambari ya simu **13 43 25 84**.

Jukumu na huduma zinazotolewa na vituo vya afya ya jamii vinachunguliwa na idara ya Afya ya Queensland. Walakini, mipango na huduma zifwatazo za afya ni mifano ya zile zinazoweza kutolewa katika maeneo tofauti.

Huduma ya afya ya watoto na vijana

Ikiwa unataka kujua zaidi kuhusu mojawapo ya huduma zifwatazo, piga simu kwa laini ya Afya ya Watoto (07) 38622333 au 1800 177 279 (nje ya Brisbane).

Huduma na kliniki za Afya ya Watoto

- Hutoa upimaji, elimu na usaidizi kwa wazazi wa watoto wenye umri wa miaka 0-12
- usaidizi wa kunyonyesha
- vikundi vya wazazi wapya na mipango ya uzazi
- kliniki za chanjo
- huduma za uhusiano wa afya (mfano. mtaalamu wa lishe, mfanyi kazi wa jamii, mtaalamu wa kiakili)
- uchunguzi wa shule ya msingi
- utembeleaji wa baadhi ya nyumba
- uchunguzi na kuhakikisha maendeleo na ukuaji wa afya ya watoto.

Huduma ya afya ya vijana katika shule

- Zinatoa miadi ya afya, makadirio, usaidizi, maelezo ya afya, uchaguzi wa rufaa pamoja na elimu na ukuzaji wa afya kwa wazazi na vijana wenye umri wa miaka 13-18 ambao wanahudhuria shule za upili za serikali

Huduma ya afya ya Akili ya Watoto na Vijana

- Hutoa mashauri, makadirio, matibabu na maangalizi kwa watoto wenye umri wa miaka 0-18 wanaoathirika na afya ya akili

Huduma za Meno zinazotolewa Shuleni

- Watoto wote wenye miaka nne na zaidi ambao bado hawajakamilisha darasa la 10 wanapewa kliniki za meno shuleni

Huduma za afya za watu wazima (kwa watu wazima wenye miaka 18 na zaidi)

Kama unataka kujua mengi kuhusu mojawapo ya huduma zifuatazo, piga simu kwa laini ya 13HEALTH, nambari ya simu 13 43 25 84. Kwa habari zaidi kuhusu huduma zinazohusiana na afya, rejelea Ukurasa wa maelezo ya 7 ya uhusiano wa Afya.

Makadirio ya kijumla ya afya, usaidizi na huduma za kliniki

- Uuguzi, huduma ya baada ya kutoka hospitali na huduma za uhusiano wa afya, pamoja na kazi za ustawi wa jamii, afya ya kazini, tibamaungo (fiziolojia) na saikolojia

Huduma ya Wazee

- Timu za uchunguzi, usaidizi nyumbani, huduma za maangalizi ya jamii na nyumba, na usaidizi ili kuboresha na kuimarisha maisha yao baada ya ugonjwa au upasuaji

Huduma za urudishaji kwa jamii

- Huduma za uhusiano wa afya (tibamaungo (fiziolojia), afya ya kazini na matibabu ya matamko/usemi)

Huduma za upunguzaji Maumivu

- (‘Upunguzaji maumivu’ inamaanisha maangalizi wa watu ambao wana ugonjwa usiotibika, ambao wanakufa.)
- kupanga huduma za upunguzaji maumivu katika jamii, maelezo na elimu na usaidizi katika msiba.

Huduma za Afya ya Akili ya Watu wazima

- Uchunguzi, matibabu na maangalizi wa watu wazima walioathirika na magonjwa ya akili

Huduma za meno ya watu wazima

- mkliniki za meno kwa watu wazima bila malipo ambao wanafikia vigezo vya kustahiki (angalia Ukurasa wa maelezo ya 6 Huduma za Meno)